Mkataba wa Afrika juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto

Mwaka wa elfu moja mia tisa na tisini, Umoja wa Afrika uliandika Mkataba wa Afrika juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto ili kuongeza ulinzi zaidi kwa haki za watoto. "Haki" ni kitu ambacho kila mtoto anastahili kupata. Haki za mtoto mmoja hazi-wezi kuondoa haki za mtu mwingine. Wakati mtoto ni mdogo, watu wazima lazima wafanye maamuzi kwa mtoto. Watu wazima wanapaswa kuzingatia juu ya kile ambacho kinafaa kwa mtoto, si kile mtoto au mtu mzima anataka. Wakati mtoto anapozidi kukomaa, ana faa apewe uhuru zaidi na ataweza kufanya maamuzi zaidi juu ya haki zake.

Mtoto ni mtu mdogo kuliko umri wa miaka 18. Watoto wote wana haki hizi, bila kujali wana-vyoonekana, wapi wanai-shi, ni dini gani au kabila gani wanapotoka, iwe ni wavulana au wasichana, au ni wazazi wao nini wana-chofanya.

Haki za watoto

Watoto wana haki ya...

· kuishi na kukua. Watoto hawawezi kuuawa hata kama wamefanya uhalifu.

· wanafaa wapate jina na nchi.

· wanafaa waseme wanacho fikiria ata kama inaudhi wengine.

· waungane pamoja katika vikundi ambazo ni za amani.

· waumini wa dini ambayo wanataka. Wazazi wanafaa kuwasaidia kujua maadili mazuri, ukweli na kisicho kuwa cha kweli.

· faragha.

· masomo ili kukuza talanta. Haya masomo yanafaa kujumuisha maadili na utamaduni wa kiafrika. Watoto wanafaa wafuzwe kuishi pamoja na watu wa tabaka na dini mbali mbali. Jinsi ya kutunza mazingira yao na kuwa na afya njema.

· kucheza na kufanya sanaa

· watoto wanafaa wapewe usaidizi maalum ili waweze kushiriki katika jamii na waweze kupata elimu wakati wana ulemavu.

· msaada wa dawa na maji safi ili waweze kuwa na afya njema.

· watoto wanafaa Kuwa na hali salama za kufanya kazi. Watoto hawafai kutumiwa vibaya wakati wanafanya kazi. Hawafai kufanya kazi ambazo huwaumiza au kuwazuia kwenda shule au kukua ki akili na mwili. Watoto hawawezi kuuzwa na mtu yeyote hata ikiwa ni wazazi wanataka. Watoto hawafai kufanya kazi kama waombaji.

· kuthibitishwa kuwa na hatia ya uhalifu. Watoto waliofanya uhalifu hawawezi kuteswa au kuwekwa na wahalifu wazima.

· watoto wanafaa kuishi na wazazi wao kama hakuna hatari. Ikiwa mtoto haishi na wazazi wake, anafaa apewe mtu na wazazi wake. Watoto hawafai kuishi gerezani kwa sababu mama yao amefungwa.

· kama watoto wametenganishwa na wazazi wao, wanafaa wapewe nyumba salama za familia mpaka watakapo ungana na famia zao.

Wajibu wa Watoto

Watoto wana majukumu kwa jamii. Wanapaswa kuonyesha heshima kwa wazee, kusaidia kuunganisha na kuimarisha Afrika, na kufanya kazi kwa amani kwa kutumia vipaji vyao.

Majukumu ya Wazee & Serikali

Sheria hii ni muhimu zaidi kuliko desturi zote na mila ambayo inakabiliana na sheria hii.

Watu wazima wanapaswa kufanya kile ambacho kinafaa kwa mtoto wakati wa kufanya uamuzi. Wanapas-wa kuomba maoni ya mtoto. Ni wajibu wa wazazi kutunza watoto wao. Wazazi na serikali lazima watunze mahitaji ya mtoto wanapokua. Adhabu haiwezi kuwa na madhara kwa mtoto.

Watu wazima na serikali lazima wawalinde watoto kutoka...

· unyanyasaji au mateso.

· mazoea ya jadi ambayo yanawaumiza watoto, kama ndoa ya watoto.

· vita. Watoto hawawezi kuwa askari au kufanya kazi katika vita.

· utunzaji usiofaa.

· unyanyasaji wa kijinsia.

· matumizi mabaya ya madawa ya kulevya na biashara ya madawa ya kulevya.

Serikali inapaswa kulinda watoto ambao wameacha nyumba zao kama wakimbizi.

Serikali na mashirika wanapaswa kupanga mpango wa watoto kwa uangalifu ili kuhakikisha kuwa watoto watakuwa salama na kupendwa katika familia zao mpya.

Child Protection Toolkit